# Umuhimu wa Kipimo cha Madini ya Risasi katika Damu ya Mtoto Wako

Kipimo cha madini ya risasi katika damu hutumika kubaini kiasi cha madini ya risasi kilicho katika damu ya mtoto wako. Madini ya risasi yanaweza kuathiri ukuaji wa mtoto, tabia na uwezo wa kujifunza. Kiwango cha chini ni bora zaidi. Hata hivyo, hakuna kiwango cha madini ya risasi ambacho kimethibitishwa kuwa salama.

Sumu ya madini ya risasi hutokea wakati watoto wanalamba, kumeza au kupumua vumbi ya rangi yenye madini ya risasi. Nyumba nyingi zilizojengwa kabla ya 1978 zina rangi ya zamani ya madini ya risasi, na mara nyingi huwa chini ya rangi mpya zaidi. Rangi ikichukuba, kupasuka au kuchakaa, vibanzi na vumbi kutokana na kwa rangi ya madini ya risasi ya zamani vinaweza kuenea kwenye sakafu, kingo za madirisha na sehemu inayoizunguka nyumba yako. Uchimbaji madini umefanywa katika sehemu kubwa ya Missouri. Viwango vya juu vya madini ya risasi katika hewa, vumbi na udongo vimepatikana katika maeneo ya karibu na migodi ya uchimbaji madini. Taka za uchimbaji madini katika maeneo haya zimetumika katika barabara za magari, nyenzo za kutupia taka, na hata katika maeneo ya kuchezea watoto. Vyanzo vingine vya madini ya risasi ni pamoja na maji ya kunywa, vito, vyombo vya udongo na mavumbi ya kazini yanayoletwa nyumbani. Rangi ya madini ya risasi, vumbi, na vifaa vingine vyenye madini ya risasi vinaweza kutua kwenye mikono ya watoto na midomoni mwao ambapo wanaimeza au kuivuta.

Watoto wengi wameguswa na madini ya risasi kutokana na rangi ya zamani, udongo, mabomba au vyanzo vingine. Watoto wote wa umri wa chini ya miaka 6 wanapaswa kupimwa ili kubaini visababishi vya hatari katika kila ukaguzi wa afya ya watoto. Ikiwa mtoto yuko katika hatari ya kuathiriwa na sumu ya madini ya risasi, anapaswa kupimwa. Watoto wote wa umri wa chini ya miaka 4 wanapaswa kupewa elimu kuhusu madini ya risasi na kupimwa kila mwaka. Kwa watoto wa umri wa hadi miaka sita, daktari au muuguzi wako anapaswa kukuuliza katika kila ziara ukaguzi wa afya ya watoto kuhusu njia ambazo mtoto wako huenda anagusa madini ya risasi. Watoto ambao wamegusa madini ya risasi wanapaswa kupimwa. Zaidi ya hayo, serikali ya Shirikisho inaagiza kwamba watoto WOTE wafanyiwe kipimo cha kiwango cha madini katika damu yao wanapopokea msaada wa Medicaid wakiwa na umri wa miezi 12 na 24, angalau.

Matokeo ya kiwango cha juu baada ya kipimo kwa kutumia damu kutoka kwenye nchi ya kidole au mguuni yanapaswa kupimwa tena kwa kipimo cha pili kwa kutumia damu iliyotolewa kwenye mshipa (mara nyingi kwenye mkono). Ikiwa matokeo ya pili bado yanaonesha kiwango cha juu, fuata hatua zilizo hapa chini.

| Matokeo ya Kipimo(mcg/dL) | Hatua Zinazofuata |
|---|---|
| **0-3.4** | • Kuna kiwango kidogo sana cha madini ya risasi katika damu ya mtoto wako.<br>• Fanya vipimo vya madini ya risasi vya siku zijazo unaposhauriwa na mtoa huduma wako. |
| **3.5-9.9** | • Hiki ni kiwango cha ya thamani ya marejeleo iliyowekwa na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC). Zungumza na daktari wako na idara ya afya ya eneo lako ili ufahamu jinsi mtoto wako huenda aligusana na madini ya risasina kupunguza uhatarisho wa mtoto wako.<br>• Daktari wako anapaswa kumpima mtoto wako tena ndani ya miezi 3. |
| **10-14.9** | • Kiwango cha madini ya risasi cha mtoto wako kiko juu.<br>• Daktari wako na wahudumu wa idara ya afya ya eneo lako watazungumza nawe ili kukusaidia kutambua vyanzo vya madini ya risasi na kupunguza uwezekanowa mgusano wa mtoto wako.<br>• Mtoto wako anapaswa kupimwa tena ndani ya mwezi 1 hadi miezi 3. |
| **15-44.9** | • Kiwango cha madini ya risasi cha mtoto wako ni cha juu kabisa.<br>• Zungumza na daktari au muuguzi wako kuhusu lishe ya mtoto wako, ukuaji na ustawi wake, na vyanzo vinavyowezekana vya madini ya risasi.<br>• Zungumza na idara ya afya ya eneo lako kuhusu jinsi ya kumlinda mtoto wako dhidi ya madini ya risasi.<br>• Mtu aliyepewa mafunzo ya hali ya juu kutoka idara ya afya ya eneo lako au Idara ya Afya na Huduma za Wazee ya Missouri (DHSS) anaweza kuzuru nyumbani mwako ili kukusaidia kutambua vyanzo vya madini ya risasi.<br>• Ikiwa kiwango cha madini ya risasi ni 15 hadi 24, mtoto wako anapaswa kupimwa tena ndani ya mwezi 1 hadi miezi 3. |

| | |
|---|---|
| | • Ikiwa kiwango cha madini ya risasi ni 25 hadi 44, mtoto wako anapaswa kupimwa tena ndani ya mwezi 1. |
| **45-69.9** | • Mtoto wako anahitaji dawa ili kumsaidia kupunguza kiwango cha madini ya risasi katika damu yake.<br>• Mtu aliyepewa mafunzo ya hali ya juu kutoka idara ya afya ya eneo lako au DHSS atazuru nyumbani mwako ili kukusaidia kutambua vyanzo vya madini ya risasi.<br>• Mtoto wako hapaswi kuwa katika chanzo cha madini ya risasi. Ikiwa chanzo hiki ni nyumbani mwako, unafaa kutafuta mahali pengine pa kuishi hadi chanzo hiki cha madini ya risasi kiondolewe au kurekebishwe. Mtoto wako anahitaji kupimwa ndani ya mwezi 1 baada ya kupewa matibabu. |
| **70 au zaidi** | • Mtoto wako anahitaji matibabu mara moja.<br>• Mtoto wako anahitaji dawa ili kumsaidia kupunguza kiwango cha madini ya risasi katika damu yake.<br>• Mtoto wako anaweza kulazwa hospitalini, hasa ikiwa kuna madini ya risasi nyumbani mwako.<br>• Mtu aliyepewa mafunzo ya hali ya juu kutoka idara ya afya ya eneo lako au DHSS atazuru nyumbani mwako ili kukusaidia kutambua vyanzo vya madini ya risasi.<br>• Inashauriwa mtoto wako asirudi nyumbani hadi vyanzo vya madini ya risasi viondolewe au kurekebishwa.<br>• Mtoto wako anahitaji kupimwa ndani ya wiki 2 hadi 4 baada ya kupewa matibabu. |

Jina la Mtoto: ________________________________Matokeo ya Kipimo: __________ mcg/dL Tarehe _____________
*Ikiwa matokeo ya kipimo hayajaandikwa hapa, muombe daktari au muuguzi wako ayaandike na kuyahifadhi kwa ajili ya rekodi zako.*

# Jinsi ya Kumkinga Mtoto Wako dhidi ya Sumu ya Madini ya Risasi

### Rekebisha rangi ya madini ya risasi inayochubua na ufanye matengenezo ya nyumba kwa njia salama.

- Hakikisha watoto wako mbali na rangi inayochubuka au kubambuka.
- Kabla ya kufanya matengenezo katika nyumba iliyojengwa kabla ya 1978, ipigie simu idara ya afya ya eneo lako ili ufahamu jinsi ya kufanya kazi kwa njia salama na kupunguza viwango vya vumbi, au uwasiliane na Mpango wa Utoaji Leseni kwa573-526-5873 au (bila malipo) 888-837-0927.
- Watoto na wanawake wajawazito wanapaswa kukaa mbali na matengenezo ambayo yanasababisha kubambuka kwa rangi ya zamani, kama vile kupiga msasa na kukwarua. Wanapaswa kukaa mbali hadi eneo hili lisafishwe kwa kutumia mbinu za kusafisha zenye unyevu na kifuta vumbi cha HEPA (sio kufagia kwa nyenzo kavu). Pia, miradi mingine ya ukarabati inaweza kusababisha kuongezeka kwa vumbi la madini ya risasi (k.m. mchanga wa vigae vya kaure). Miradi yote ya ukarabati inapaswa kufanywa kwa uangalifu ili kuhakikisha kuwa hakuna ongezeko la hatari ya madini ya risasi.

### Osha vumbi kwenye mikono, midoli, chupa, madirisha na sakafu.

- Mnawishe mtoto wako mikono na umuoshe uso baada ya kucheza, kabla ya kula na kabla ya kulala.
- Osha vifaa vya kuchezea, midoli iliyojazwa, minyonyi na chupa za watoto kwa sabuni na maji mara nyingi.
- Safisha sakafu mara nyingi, na utumie vipanguzaji vya karatasi vyenye unyevunyevu kusafisha kingo za madirisha.

### Kuwa mwangalifu usilete vumbi la madini ya risasi nyumbani kupitia nguo, midoli au vito.

- Madini ya risasi yapo katika baadhi ya vito vya watoto, midoli, funguo na samani kuukuu. Jisajili upokee arifa za kurejeshwa kwa bidhaa za watoto kwenyewww.cpsc.gov/Recalls.
- Baadhi ya kazi na burudani zinaweza kuhusisha kugusana na madini ya risasi. Hizi ni pamoja na uchimbaji madini, utengenezaji betri, upakaji rangi, ujenzi wa mabomba, ujenzi wa nyumba, ukarabati wa magari, au kutumia bunduki, vioo au vyombo vya udongo. Ili kupunguza vumbi la madini ya risasi, badilisha mavazi ya kazini kabla ya kwenda nyumbani; vua viatu ukiwa mlangoni mwako; osha mavazi ya kazi au burudani kando na mengine; osha uso, mikono na ngozi isiyofunikwa na mavazi kabla ya kwenda nyumbani.

## Zuia madini ya risasi kuingia katika chakula chako na maji ya bomba.

- Ikiwa una mabomba yaliyotengenezwa kwa madini ya risasi, yatiririshe maji ya bomba yakiwa baridi kwa dakika moja kabla ya kuyatumia, ikiwa hayakuwa yakitiririka saa kadhaa. Maji ya jiji na kisima yanaweza kuwa na madini ya risasi kutokana na mabomba ya zamani.
- Tumia tu maji baridi ya bomba kwa kunywa, kupika na kuandaa chakula cha watoto. Kuchemsha maji *hakuondoi* madini ya risasi. Badala yake, viwango vya madini ya risasi vinaweza kuwa vya juu zaidi kutokana na viwango vya juu vya uvukizi.
- Tumia vyomba vya kulia visivyo na madini ya risasi. Usipakue chakula au kukihifadhi kwenye mabati, jiwe la kioo au vyombo vya udongo vilivyopasuka. Vyakula vyenye asidi, kama vile nyanya na juisi ya machungwa, vinaweza kuyeyusha madini ya risasi kwenye vyombo vya kuhifadhia.
- Tembelea tovuti zilizo hapa chini ili ufahamu sahani, viungo, peremende, vipodozi na tiba za afya ambazo zimetambuliwa kuwa na madini ya risasi.

## Pakua vyakula vilivyo na kalsiamu, madini ya chuma na vitamini C.

- Vyakula hivi husaidia kuzuia madini ya risasi kuhifadhiwa katika mwili wa mtoto wako.
- Vyakula vyenye kalsiamu: maziwa, jibini, mtindi, tofu, mboga za kijani kibichi.
- Vyakula vyenye chuma: maharagwe, nyama konda, nafaka asili, siagi ya karanga.
- Vyakula vyenye vitamini C: machungwa, juisi ya machungwa, zabibu, nyanya, pilipili hoho.

## Pata maelezo zaidi kuhusu madini ya risasi.

- Zungumza na daktari au muuguzi wa mtoto wako.
- Ipigie simu idara ya afya ya eneo lako. Ili kutazama orodha: www.health.mo.gov/living/lpha/lphas.php.
- Tembelea tovuti ya Idara ya Afya na Huduma kwa Wazee katika Missouri: www.health.mo.gov/living/environment/lead/.

Maelezo haya yametolewa kwenye Idara ya Afya ya Jimbo la New York, Chapisho la 2526

MISSOURI DEPARTMENT OF HEALTH & SENIOR SERVICES